

**HOTUBA YA MGENI RASMI HENRY BANTU KAIMU MWENYEKITI
WA BODI YA WAKURUGENZI MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI
ARDHINI KATIKA**

**UZINDUZI WA JUKWA LA WANAFUNZI – UNIFORUMU – TAWI LA
LATRA CCC CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM JUMAMOSI**

TAREHE 26 JUNI, 2021

**Prof. Willyam Anangisye - Makamu Mkuu wa chuo Kikuu cha
Dar Es Salaam,**

**Mama Paulina Mabuga Dean wa Wanafunzi, Chuo Kikuu cha Dar
es Salaam**

Bw. Ebenezer Mshana, Mlezi wa Wanafunzi – UNIFORUM,

Bw. Gilliard Ngewe, Mkurugenzi Mkuu LATRA,

**Dr. Makuke Mwenyekiti wa Baraza la Watumiaji Huduma za
Usafiri Ardhini,**

**Bw. Godwell Paulo Rais wa Wanafunzi Pamoja na Viongozi
Mbalimbali wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es
Salaam,**

**Viongozi Mbalimbali wa Serikali na Taasisi Binafsi walioalikwa,
Wanachama wote wa Jukwaa la Wanafunzi – UNIFORUM –
Waandishi wa Habari, Mambibi na Mabwana,
Nawasalimu kwa Jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**

Awali ya yote, ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha sote kufika hapa kutoka sehemu mbali mbali, tukiwa ni mashuhuda wa safari ndefu ya kuanzishwa Jukwaa la kujadili mambo muhimu katika Sekta ya Usafiri Ardhini- UNIFORUM-LATRA CCC – Tawi la Chuo Kikuu Dar es Salaam. Natoa shukrani zangu za dhati kwa waandaaji wa Shughuli hii ya ufunguzi na kwa kunipa heshima ya kuwa Mgeni Rasmi katika uzinduzi huu wa leo na kwa mapokezi na maandalizi mazuri yaliyofanyika.

Aidha, ninapenda kuwashukuru wote mlionhudhuria, kushiriki sote katika Uzinduzi huu wa Kihistoria katika chuo chetu. Bila shaka mnazo shughuli nyingine nyingi mlizoziacha kwa ajili ya kuhudhuria Uzinduzi huu. Kufanya hivyo, kunatokana na umuhimu mlipoa shughuli ya leo, hapa Chuoni. Kuwepo kwenu hapa ni faraja kubwa kwangu na kwa wanafunzi wote na memba wa Jukwaa hili.

Ahsanteni sana.

Kifungu namba 31(1) (e) cha Sheria namba 3 ya LATRA ya Mwaka 2019, kinatoa wajibu kwa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini (LATRA CCC) kuanzisha na kusimamia Kamati au Majukwaa ya Watumiaji kwenye maeneo shule za Msingi, Sekondari na Vyuo Mbalimbali Nchini. Lengo likiwa ni kuwapa fursa watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini kupata mahali pa kujadili na kutatua matatizo mbalimbali katika Sekta. Kwa namna ya Pekee sana, Nishukuru Uongozi wa Chuo kwa kukubali kwao, kuanzishwa kwa Tawi hili.

Aidha; Niwashukuru kwa namna ya pekee, Viongozi wote wa UNIFORUM kwa kumpokea aliyejekuwa Katibu Mtendaji wa Baraza, Dr. Oscar Kikoyo ambaye Sasa ni Mbunge Wa Muleba alipokuja kwa mara ya kwanza hapa chuoni kuleta habari hizi Mwaka 2019. Msingempokea leo hii, tusingeweza kufanya jambo hili la kihistoria. Aidha, nimshukuru pia, Rafiki yetu, kiongozi wetu, mshauri wetu, Bw. Ebeneza Mshana. Yeye amekuwa mstari wa mbele na bila kuchoka, kuongoza wanafunzi mpaka kufanikiwa, kusajili Jukwaa hili. **Asante sana.**

Kama nilivyosema awali, Jukwaa hili ni chombo muhimu cha kuwaunganisha wadau mbalimbali katika kujadili na kuweka mikakati mbalimbali ya kutatua changamoto za Usafiri katika chuo chetu au sehemu mbalimbali Nchini. Ninafahamu kuwa, Sheria imetoa majukumu kadhaa kwa Baraza. Miongoni mwa majukumu hayo ni pamoja na;

- (i) Kuwakilisha maslahi ya watumiaji wa huduma za usafiri kwa njia ya Reli, usafiri wa umma kwa njia ya barabara, usafiri wa chini ya ardhi na usafiri kwa njia ya waya, kwa kuwasilisha, kupata maoni na tarifa na kwa kushauriana na Mamlaka, Waziri mwenye dhamana na wadau wa sekta mbalimbali zinazodhibitiwa;
- (ii) Kupokea na kusambaza tarifa na maoni mbalimbali kuhusu masuala yanayowagusa watumiaji wa huduma zinazosimamiwa na LATRA;
- (iii) Kuunda kamati za Watumiaji wa huduma za usafiri wa Sekta zinazodhibitiwa na LATRA katika Mikoa na Kushauriana nazo;
- (iv) Kushauriana na wadau , Serikali na makundi ya watumiaji kuhusu huduma;

- (v) Kufanya utafiti juu ya maslahi, haki, wajibu na masuala mengine yanayogusa watumiaji.

Ni kwa kutumia Jukwaa hili, Wanafunzi wote wanapata fursa ya kuwasilisha maoni yao kwa uhuru na kuleta mabadiliko chanya katika Sekta. Hasa wanafunzi mnawenza kujikita katika maswala ya Utafiti katika Sekta ya Usafirishaji.

Ndugu Wanachuo na wageni waalikwa,

Wakati wa taarifa yenu ya utendaji wa TAWI la UNIFORUM kwa kipindi cha mwaka mmja uliopita, mmetaja mafanikio kadhaa pamoja na changamo. Nimende tu kusema, changamoto mlizopitia ni chachu ya kuwa na Jukwaa, bora Zaidi. Kwa maeneo ambayo mmeleta mapendeleko yenu, napenda kuyatolea ufanuni na majibu kama ifuatavyo:

- 1) Kuwa na mafunzo kwa wanachama ili wapate ufahamu na uelewa kuhusu LATRA na LATRA CCC na shughuli zake kupitia semina mbalimbali na makongamano. Hapa ninaagiza Baraza, kuanzia sasa na kuendelea, kuwa karibu na Jukwaa hili katika kutoa elimu mbalimbali ikiwemo:
 - (a) Umuhimu wa abiria kutumia teknolojia ya kielektroniki kukata tiketi za mabasi yote ili kupunguza gharama na kuendena na mazingira ya sasa.

- (b) Kuelimisha umuhimu wa abiria kukemea mwendo kasi na matumizi sahihi ya mfumo wa ufuatiliaji mwenendo wa mabasi Nchini unaosimamiwa na LATRA pamoja na
- (C) Kuwasaidia wanafunzi kufanya tafiti mbalimbali katika Sekta zitakazo leta mapinduzi ya maendeleo Nchi.
- 2) Kupata vifaa vyaa kisasa vyaa kielektroniki kama vile kompyuta yaani PC au IPAD kwa ajili ya kurahisisha shughuli za UNI-FORUM. Ombi hili nimelichukuwa, na nitamwomba Mkurugenzi wa LATRA aseme Juu ya Hili.
- 3) Ombi la kupata vitambulisho pamoja na kutenga Bajeti kwa ajili ya Tawi hili, ninaagiza Uongozi wa Baraza ukae na uongozi wa Jukwaa hili ili kuona namna bora ya kutekeleza maombi haya.

Ndugu Wanachuo, na wageni waalikwa,

Nimefahamishwa, Pia kuwa, Wapo wanachama wa UNIFORUM waliohitimu masomo yao mwaka jana na Wapo wanaohitimu masomo yao mwaka huu. Niwapongeze sana kwa hatua hii muhimu na niwajulishe kuwa, Endapo Mkiona nafasi za Kazi za LATRA na LATRA CCC msisite kuomba nafasi hizo. Aidha, kwa wanafunzi wanaoendelea na masomo yao ninawasihi kuongeza bidii katika

masomo yao ili tuzidi kupata wataalam sahihi kwa ujenzi wa Taifa letu.

Ndugu Mkuu wa Chuo, wahitimu na wageni waalikwa,

Napenda kuwaaga wahitimu kwa neno maalumu la kuwausia mnapoondoka hapa, mfahamu bayana kuwa popote mtakapokuwa na kwa wadhifa wowote mtakaokuwa nao, msisahau kwamba matendo yenu, tabia yenu na hekima zenu zitakuwa ni kioo na taswira ya Chuo na Jukwa hili la UNIFORUM. Watu watapima hadhi ya Chuo hiki na mafunzo yanayotolewa hapa kwa kuwatazama jinsi mnavyozimudu shughuli zenu za kazi na kwa mienendo yenu ya maisha. Kwa hivyo deni lenu la fadhila ni kuwa mabalozi wazuri wa Chuo hiki na Jukuwaa hili huko mwendako, na daima muenzi elimu mliyopata hapa.

Mwisho kabisa nawatakia wote kila la kheri katika maisha,

Asanteni Sana.